

Angelika Dahlin – Pumzika kwa amani!



Bibi Angelika Dahlin (1953-2021) ametuachia pengo lisilozibika na majonzi makubwa. Hata hivyo, kupitia kwake tumejifunza mambo mengi hasa ukarimu, kuwapenda na kusaidia wenzetu wenye matatizo. Pia kutokukata tama na kupambana wakati wote. Hakutaka mtu kuonewa wala hakupenda kuonea watu. Alikuwa mkweli daima.

Alikuwa ni mmoja kati ya wafadhili wakubwa wa jitihada za kutokomeza ukeketaji, ndoa za utotoni pamoja na aina zote za ukatili Tanzania kupitia mashirika ya NAFGEM Tanzania na Tanga Inter- Africa Committee (TIAC).

Yeye na mumewe Dr. Claes Göran Dahlin walikutana Tanzania wakati wa ujana wao, wakaoana na kufanya kazi katika hospitali ya Lugarawa, Iringa.

Bibi Angelika alikuwa na mapenzi ya dhati kwa NAFGEM Tanzania ambayo aliichukulia kama ni moja kati ya shughuli zake za kipaombele. Aliwapenda sana wanawake na watoto hasa walioko kwenye mazingira hatarishi. Alitafuta raslimali za kuwasaidia kwenye nyanja mbalimbali ikiwa ni pamoja na elimu, huduma za afya, kuwatambua na kuwasaidia watoto wanaoishi kwenye ulemavu.

Kwa kutumia Ki-Swahili ambacho walikimudu na kukipenda sana, waliweza kuwafikia na

kuzungumza na walengwa wa huduma za NAFGEM Tanzania kwenye maeneo mbalimbali. Alijua sana Simanjiro, Hai, Siha, Kilimanjaro, Moshi vijijini, Pangani na Duga Maforoni.

Kwa ujumla, Angelika Dahlin aliigusa mioyo ya wanawake na watoto wengi sana ambao watamkumbuka sana. Bibi ataishi milele kwenye nyoyo za jamii nyingi alizozigusa kwa namna moja au nyingine.

NAFGEM Tanzania inaomboleza na kusikitika sana. Hata hivyo, tunashekea sana maisha yake aliyoyaishi hapa duniani. Tunaishukuru sana familia yake na hasa Babu Claus na watoto wake ambao walikuwa sehemu ya maisha yake ya kila siku. Tunalishukuru pia shirika la Network Rafael ambao walimwamini na kumsikiliza sana Angelika kwa niaba ya NAFGEM Tanzania.

Pumzika kwa amani, mama na rafiki wa kweli.

Raha ya milele umpe eeh bwana, na mwanga wa milele umwangazie, amina!